

Muwe na Imani Pamoja

Ni rahisi kusikia hadithi kwenye Biblia au kutoka kwa watu wanaomfuata Yesu leo na kufikiri, "Sitawahi weza kufanya kitu kama kile."

Waebrania 11:1, 6 Inasema, "Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo na bayana ya mambo yasiyoonekana... Na pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu, kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yupo na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao."

Waebrania 11 Inaeleza kuwa mojawapo ya viungo muhimu katika kumtumikia Mungu ni kuwa na 'imani'. Miongoni mwa mengine mengi inazungumzia kuhusu Nuhu na Ibrahimu, wayahudi wawili 'mashujaa' waliomfuata Mungu. Hadithi zao zipo kwenye Agano la Kale.

Tunapata hadithi ya Nuhu katika Mwanzo 6 inasema, "Nuhu alitenda kila kitu sawa na vile Mungu alivyomwamuru." Mungu alitaka kutuma mafuriko ilhali alitaka kuwaokoa wale waliomwamini. Alimwagiza Nuhu kujenga meli mahali ambako hapakuwa na maji! Hebu tafakari hayo! Watu walimdhahiki Nuhu na kumuona ana wazimu. Maji yalikuja na watu wote walikufa isipokuwa Nuhu na jamii yake. Imani ya Nuhu kwa Mungu iliokoa maisha yake.

Ibrahimu yuko tofauti (Mwanzo 12-25). Ibrahimu aliambiwa na Mungu kwamba atapata mtoto wa kiume ijapokuwa alikuwa mzee na Sara hangeweza kupata watoto. Sara hakuamini kamwe. Alicheka Ibrahimu alipomwambia Mungu alimwambia Ibrahimu kwamba wazao wake watakuwa wengi kama nyota. Ibrahimu aliona ugumu kuamini. Mwishowe licha ya ugumu huu Mungu aliwapa Ibrahimu na Sara mtoto na kutimiza ahadi yake kwao. Waebrania 11 inasema kwa imani Ibrahimu na Sara walipata mtoto!

Imani hupimwa kwa matendo-huonekana kwa jinsi tunavyoishi. Hii ina maana kuwa tunapaswa kufanya kile ambacho Mungu anatuagiza tufanye hata kama hatuelewi sababu kikamilifu! Iwapo Mungu amesema atapeana mahitaji yetu au kutulinda, imetupasa kuamini hivyo na kwa kuzingatia tufanye kushinda uoga wetu. Imani ni kuweka matarajio yetu kwa Mungu kutenda katika hali zaidi ya uwezo wetu wenyewe. Tunapoamua kuweka imani yetu kwa Mungu, tunaamua kumwamini Mungu mwenyewe, neno lake (Bibilia), na katika utendakazi wake kati ya maelfu ya watu. Mungu anaweza kutenda zaidi ya tunavyoweza kuomba au kuwaza.

Zingatia!

Je Mungu anakuhimiza ufanye nini? Mwezi uliopita tuliangalia jinsi ya kuanzisha Kikundi cha Uzima. Je tunahitaji kuweka imani yetu katika matendo ili kuanza? Kujipeana 'kule nje' kwa umma? Je Mungu anatumiza kumweleza Yesu kwa watu ama kutafuta pesa kumsaidia mtu? Bila imani haiwezekani kumwamini Mungu. Amini. Tenda. Ona kile Mungu anafanya!


Omba:

- 1) Mungu atakupa imani kubwa zaidi na kukuonyesha jinsi ya kuiweka katika matendo (Waefeso 2:8-10).
- 2) Shaka na hofu zozote ulizonazo utazishinda unaposoma Biblia na kusikiza neno la Mungu juu ya maisha yako.



Bernard aliomba na Petro, aliyekuwa amevunjika moyo baada ya kumpoteza mkewe. "Tulipokuwa tukiomba nilihisi kitu kama upepo mkali... Hapakuwa na upepo uliovuma, lakini nilihisi upepo mkali. Baada ya hapo nimeanza kujihisi kuwa mwepesi, kana kwamba nilikuwa nimefungwa na sasa nimeachiliwa."

- Bernard & Peter*, Kalweo, Zambia



Funzo hili limechochewa na "Imani-Twahitaji Kuamini" funzo katika Kupenda Kijiji Chako, kitabu kinachowasaidia watu kuwatumikia wengine kwa ujumbe wa Yesu. Kwa maelezo zaidi:

dignityonline.org.uk/publications